# Uzima na heri kwenu - Zb 68(69)

12 è DTO-A

Muziki : Toni Iragi K




1.Ee Bwana, kwa ajili yako ninavumilia feze**ha**,
haya imenifunika uso wa**ngu.**
Maana juhudi ya nyumba yako imenimali**za,**
na matukano yao wanaokutukana wewe yamenipa**ta.**

2.Nami, sala yangu inakuelekea, ee Bwa**na,**
wakati wa neema yako, ee Mu**ngu:**
Unisikilize kwa wema wako mku**bwa,**
kwa uaminifu wa wokovu wa**ko.**

3.Nami, niliye mnyonge na mgo**njwa,**
ee Mungu, msaada wako unili**nde!**
Nitalisifu jina la Mungu kwa wi**mbo,**
nitamtukuza kwa kumtolea shukra**ni.**

4.Enyi wanyonge, tazameni, furahi**ni,**
enyi mnaomtafuta Mungu, moyo wenu ufufu**ke.**
Kwa maana Bwana huwasikia maski**ni,**
wala hawazarau wafungwa wa**ke.**